# Same and Mwanga Environmental Conservation Advisory Organization (SMECAO)

TOLEO LA KWANZA

JULAI, 2011

# TUBADILIKE!



SMECAO FUND,
P.O BOX 87,
SAME - KILIMANJARO,
Email: smecao@gmail.com,
smecao@elct.org,
Website: www.smecao.jimdo.com

## Safu ya wafanyakazi Same and Mwanga Environmental Conservation Advisory Organization (SMECAO)



Bibi Veneranda Sachore,
Mkurugenzi wa SMECAO



Bibi Lenna Msuya,
Mratibu



Paul Peter Nyindo,
Mkuu wa Idara ya
Afya na Ukimwi



Susan G. Kagize,
Mkuu wa Idara ya
Ujasiriamali na Usawa wa
Jinsia



Alphonce Sambura,
Mkuu wa Idara ya
Mazingira na Mabadiliko
ya Tabia Nchi



Benard W.Mkwizu,
Mkuu wa Idara ya Sheria
na Haki za Binadamu



Vedasto Sukumu,
Mfanyakazi wa kujitolea
Kutoka WWF Tanzania
katika program ya YETS.



Jens Oke Johansen
Mfanyakazi wa kujitolea



Lukas Jeremia,
Dereva

# SALAMU TOKA KWA MKURUGENZI



**Bibi Veneranda Sachore,**
**Mkurugenzi wa SMECAO**

SMECAO (Same and Mwanga Environmental Conservation Advisory Organization), ni mradi ulioanzishwa mwaka 1994 na marehemu ndugu Saimon Emanuel Mmakasa chini ya mwamvuli wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Pare .

Mwaka 1999 SMECAO iliandikishwa kama shirika lisilokuwa la kiserikali (NGO) na linaongozwa na Bodi yenye wajumbe nane.

Shirika linafanya kazi katika eneo la wilaya za Same na Mwanga mkoani Kilimanjaro.

Shughuli kuu ni pamoja na kuelimisha jamii juu ya mabadiliko ya tabia nchi na uhakika wa chakula, elimu ya mazingira na utumiaji wa nishati jadidifu, Haki za binadamu na Jinsia, Ujasiriamali na Elimu ya Ukimwi kwa jamii.

Kwa kipindi cha mwaka 2010/2013 shirika linafanya kazi katika kata nne; nazo ni Ngujini na Kwakoa kwa wilaya ya Mwanga na Kihurio na Videe kwa wilaya ya Same.

Jarida hili limeanzishwa kwa lengo la kutoa elimu ya Ukimwi katika shule za sekondari kupitia visa na mikasa na matukio mbalimbali yanayojitokeza katika jamii yetu.

Walengwa wakuu wa jarida hili ni wanafunziwa shule za sekondari wake kwa waume, utoaji wa elimu kupitia jarida hili unalenga umfanya mwanafunzi kubadili tabia hatarishi zinazopelekea kupata virusi vya ukimwi.

Na pia kupunguza unyanyapaaji kwa wale walioathirika na virusi vya ukimwi, pamoja na walengwa wakuu kuwa ni wanafunzi wa shule za sekondari, pia linatoa ujumbe kwa wazazi kuweza kuona ni mazingira gani ambayo watoto wao wanakumbana nayo na hivyo kuweza kukabiliana na mazingira hayo.

Pia litaweza kutoa habari kwa jamii ni kwa jinsi gani wazazi au watu wazima wanavyoweza kuchangia kumwingiza mwanafunzi katika tabia hizo hatarishi zinazochochea maambukizi ya virusi vya ukimwi.

Jarida hili ni jipya na la kwanza kutolewa kwa mwaka huu wa 2011, inawakaribisha wanafunzi wote kuchangia katika kutoa makala,kisa mkasa au matukio ya kweli yanayojitokeza katika mazingira wanamoishi iwe shuleni au majumbani ambayo yanachangia kuenea kwa virusi vya ukimwi.

Ndugu wasomaji, karibuni tusome jarida hili na tuwe na mtazamo chanya wa jinsi ya kujihami na kuzuia maambukizi ya virusi vya ukimwi.

**PAMOJA TUTASHINDA!**

**Karibuni na Asanteni**

# HISTORIA YA ASASI HII (ORGANIZATION PROFILE)

**Na Paul Nyindo,**
**Idara ya Afya na Ukimwi**

SHIRIKA la ushauri la uhifadhi wa mazingira Same na Mwanga (SMECAO), lilianzishwa mwaka 1994 likiwa chini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Dayosisi ya Pare.Shirika Limefanyakazi katika wilaya za Same na Mwanga mkoani Kilimanjaro.



**Bibi Veneranda Sachore,**
**Mkurugenzi wa SMECAO**

SMECAO linatekeleza shughuli zake kwa kuijenga uwezo jamii katika programu zinazolenga mabadiliko ya tabia nchi ,utunzaji wa mazingira,Haki za Binadamu na usawa wa kijinsia, uzalishaji /ujasiriamali na ukimwi na afya,katika kata za Kihurio na Vudee wilayani Same na Ngujini na Kwakoa wilayani Mwanga.

SMECAO imesajiliwa chini ya Bodi ya udhamini mwaka 1998 na sasa shirika linaongozwa na bodi ambayo ina wajumbe nane ambao Mwenyekiti wake ni Augustino Kessy. Shirika linafadhiliwa na Bread for the World (BFW) toka Stuttqart – Ujerumani.

Shirika lina wafanyakazi saba,ambao Mkurugenzi wake ni Mrs.Veneranda Sachore, Mratibu ni Mrs Lenna Msuya, Paul Peter Nyindo Idara ya Afya na Ukimwi,

Benard W. Mkwizu Idara ya Sheria, Haki za Binadamu,Suzan G. Kagize Ujasiriamali na Usawa wa Jinsia, Alphonce Sambura Idara ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi na Lukas Jeremia Dereva.



**Bibi Lenna Msuya,**
**Mratibu**



**Paul Peter Nyindo,**
**Idara ya**
**Afya na Ukimwi**

Pia shirika lina wafanyakazi wa kujitolea (Volunteers) ambao ni Jens Oke Johansen kutoka WELT WARTS project ya Ujerumani na Vedasto Sukum kutoka WWF Tanzania katika program ya YETS.

Vilevile Idara ya Ukimwi na Afya imefanya mafunzo ya uhamasishaji juu ya mapambano dhidi ya UKIMWI hadi sasa vijiji sita (6) ambavyo ni Kwakoa, Vudee, Ngulu, Toloha, Menamo na Kisesa vimeshafikiwa, idadi ya watu 368 wamepata mafunzo hayo.

Hamasa dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI inaendelea kufanyika kupitia sanaa shirikishi katika matamasha, kongamano na maadhimisho mbalimbali katika vijiji vyote katika kata nne.



**Benard W.Mkwizu,**
**Idara ya Sheria na**
**Haki za Binadamu**

# ATHARI ZA MAZINGIRA NA MAAMBUKIZI YA UKIMWI

**Na Alphonce Sambura,**

**Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi**

ASILIMIA kubwa ya nishati ya kupikia vijijni ni kuni, wahusika wakuu katika utafutaji wa nishati hii ni akina mama na watoto wa kike kutokana na utamaduni wetu.

Kutokana na ongezeko la mahitaji ya nishati hii, imepelekea mapori na misitu kupungua kiasi kwamba inabidi kusafiri umbali mrefu ili kujipatia kuni.

Mfano kutokana na kupanuka kwa miji ya Hedaru, Makanya wilayani Same na mengine inabidi kutembea umbali wa kilomita 4-6 na kuchukua muda mwingi kukusanya nishati hii.

Kutokana na umbali huu inabidi akina mama kujihimu alfajiri na mapema na matokeo yake muda na umbali unaotumika katika kupata nishati hii uwaweka katika hatari ya kubakwa na hatimaye kupata maambukizi ya virusi vya ukimwi.

Kwa mfano katika miaka ya tisini kumekuwa na ongezeko la matukio ya ubakaji katika mapori ya Hedaru.

Mabadiliko ya tabia nchi yamekuwa ni changamoto kwa maambukizi ya ukimwi. Hali ya ukame,upungufu wa uzalishaji katika shughuli za kilimo umepelekea kuwepo kwa misafara ya kwenda katika miji ya Ndungu, Kihurio, Hedaru, Makanya na Same kujitafutia riziki, ambayo imekuwa na ongezeko la watu kwa madai ya kutafuta ajira.

Kutokana na kiwango kidogo cha elimu, ajira rahisi imeonekana ni uuzaji wa baa pamoja na ajira kwenye nyumba za wageni hasa hasa kwa wasichana wadogo.

Kutokana na kipato kidogo wanacholipwa wanashindwa kujikimu kimaisha hivyo kujiingiza katika biashara ya ukahaba na hivyo kuwapelekea kuwa katika hatari kubwa ya maambukizi.

Kutokana na miji hii kuwa kando kando mwa barabara ya Dar es Salaam –Arusha, malori mengi yamekuwa yakiegeshwa usiku kucha na hivyo kufanya biashara ya ukahaba kushamiri na kuwaweka wasichana/akina mama katika hatari ya maambukizi.

Uharibifu wa mazingira umewafanya wanaume kuhama nyumba zao na kwenda kutafuta vibarua sehemu zenye unafuu. Kutokana na hali ya kukaa mbali na wenzi wao imewaweka katika hatari ya maambukizi na pindi wanaporejea vijijini huwa chanzo cha maambukizi kwa wenzi wao.



*Mama akitafuta kuni*

# SIKU YA KWANZA KUONA NGUJINI



**Na Suzan Kagize,**
**Usawa wa Jinsia**

MARA nyingi nimekua nikisikia msemo wa tembea uyaone, na kweli nimeyaona,siku yangu ya kwanza kuiona kata ya Ngujini ilikuwa siku ya Jumanne majira ya saa nne asubuhi, tulipoanza safari ya kuelekea maeneo ya kazi.Na usafiri mkubwa tuutumiayo kwenda maeneo yetu ya kazi ni pikipiki kwa maana hiyo inabidi uwe umejiandaa haswa, kiroho na kimwili.

Tukiwa njiani /barabara kuu kuelekea wilayani Mwanga, tulipita baadhi ya maeneo ya wilaya ya Same ambako mandhari yake ni kame sana kiasi cha kunifanya nitafakari tumeitendea nini dunia hii sisi binadamu.

Hivi ni kwamba uwezo wetu wa kudhibiti hali hii ya ukame imefika kikomo? Kutafakari huku kuliishia kwa kukosa jibu kwani sikujua nimwulize nani anisaidie.

Cha ajabu tulipoanza tu kuingia wilaya ya Mwanga hali ya hewa na madhari ilibadilika kabisa, kulikuwa na kijani cha kupendeza, hali hii inaweza kukufanya umtukuze Mungu kwa uumbaji wake madhubuti, ndipo hapa nikapata jibu la tatizo la wilaya yetu ya Same ya kuwa hali hii inaweza kubadilika kwani uwezo tunao.

Tulipofika kijiji cha Ngujini, kwa ajili ya mkutano wa hadhara tulipokelewa na kulelekezwa katika ofisi za kijiji na baadaye kwenye mkutano, Msemaji wa kwanza alipoanza kutoa mada za maendeleo niligundua ya kuwa wanawake walikuwa hawaongei na vijana walikuwa wachache sana kwenye mkutano huo.

Nikaanza tena kutafakari hivi serikali ni wakina nani? Sisi wananchi ndio chanzo cha serikali hii kwa hiyo kwanini wanawake hawa ambao ni sehemu ya serikali sauti zao hazisikiki, wanawake hawa nani atawaongelea au wanasubiri Mungu atume Mtume kuwaongelea matatizo yao.

Kingine kilichoniumiza ni uwepo mdogo wa vijana, jamii gani hii tunataka iwe na maendeleo pasi vijana kuhusika, Je, Msemo msemao vijana ni nguvu ya taifa la leo hauna tija. Je, Taifa letu litajengwa na nani? Jamani vijana tunaelekea wapi?

Nilitafakari sana, kuhusu sisi vijana hivi uzalendo wetu upo wapi. Hii inajumuisha hata sisi vijana tuliopo shuleni kwani tuna nafasi kubwa kuchangia katika maendeleo ya vijiji vyetu.

Hebu tujiulize tumelifanyia nini taifa letu kama hauna ulichofanya hustahili kuitwa Mtanzania.

Jamani wanawake tuamke, tujitahidi sauti zetu zisikike, hakuna haja ya kuwezeshwa kama sisi wenyewe hatuwezi kujiwezesha, jamani sisimizi ni kiumbe mdogo sana lakini ana uwezo wa kumwangusha Tembo, tukiamua yote yanawezekana.



*Wahitimu (TOTs) walipokua katika mafunzo yao ya UKIMWI*

## VISA na MIKASA

## VISA HIVI VIMEANDALIWA NA WANAFUNZI WA SHULE YA SEKONDARI KINDOROKO WILAYANI MWANGA (LIFE EXPERIENCE ON HIV/AIDS)

MIAKA kadhaa iliyopita palikuwa na wanandoa Bwana na Bibi Shirima waliokuwa wakiishi mkoani Arusha eneo la Ngaramtoni, katika maisha yao walipata mtoto waliemuita Andrew. Andrew alikuwa na kuanza shule lakini maisha ya wazazi wake yalianza kubadilika baada ya Bwana Shirima kuanza kutumia vilevi na kurudi nyumbani nyakati za usiku.

Pamoja na hilo mke wake aliendelea kumjali na kumtunza na baada ya mwaka mmoja waliweza kupata mtoto mwingine waliyemuitwa Aneth. Aneth alikuwa mwenye afya njema, pia Andrew alikuwa darasa la pili.

Maisha yao yalikuwa mazuri na ya furaha ingawaje tabia ya baba yao haikumpendeza mkewe na watoto.

Ghafla sana afya ya baba Andrew ilianza kubadilika na kushambuliwa na magonjwa mbalimbali ikiwemo kukohoa kupita kiasi.

Jambo hilo lilimpa mawazo sana mama Andrew kwa kuwa baba Andrew ndiye mtu pekee waliyekuwa wakimtegemea, ila alijipa matumaini kuwa mumewe ipo siku atapona.

Baba Andrew aliendelea kuzunguka huku na kule kutafuta ni ugonjwa gani ulikuwa ukimsumbua na ndipo alipobaini kuwa alikuwa akisumbuliwa na ugonjwa wa UKIMWI, ilimshtusha sana na kuanza kujutia vitu vingi na hivyo kukosa amani na aliwaza kuwa hata mkewe na watoto wote watakuwa wameathirika ingawaje alijua yeye ni muathirika ila hakutaka mke na watoto wake kugundua jambo hilo.

Wakati huo alikuwa akifuata ushauri wa daktari na hivyo afya yake ikabadilika na kurudi kama kawaida.

Siku moja usiku Bwana Shirima aliamua kutoroka bila kumtarifu mkewe na watoto kwani alihisi akiendelea kukaa pale watagundua kuwa yeye ni muathirika, asubuhi yake mkewe alikuwa mnyonge na aliita huku na kule kuuliza kama kuna mtu amemuona mumewe, huku Andrew alionekana akienda shule kama kawaida na Aneth alikuwa nyumbani.

Maisha yao yalianza kuwa magumu kwani waliishi kwa kuombaomba jambo ambalo lilimpelekea Andrew kutokusoma kwa amani na hata kushuka kimasomo.

Siku zilivyozidi kwenda mawazo yalimuandama mama Andrew na kuanza kuumwa sana hali iliyosababisha Andrew kuacha shule ili kuweza kumuhudumia mama yake mpendwa pamoja na mdogo wake.

Jambo lile liliwaumiza majirani na ndipo wakaamua kumsaidia Andrew kwa kumpeleka hospitalini mama yake na katika vipimo vilionyesha kuwa ameathirika lakini alipewa ushauri ambao ungemsaidia sana ila ushauri ule hakuweza kuutumia kutokana na mawazo yalizidi na kusema kuwa mumewe alijijua na ndio maana alimkimbia.

Afya yake iliendelea kuwa mbaya na pia watoto wake walianza kushambuliwa na magonjwa kwani walikuwa wanapata chakula kwa shida sana.Majirani waliendela kumpa moyo na kumsaidia chakula ila afya ya watoto ilizidi kuwa mbaya ndipo majirani hao waliamua kuwapeleka hospitalini ili kuwapima, ambapo Andrew alikuwa mzima huku Aneth aligundulika kuwa virusi vya ukimwi.

Majirani hawakumueleza Aneth bali mama yake ambaye alionekana kukosa matumaini na hali yake kudhoofu na alifariki siku moja usiku wa manane.

Asubuhi yake ndugu,jamaa na marafiki walifika kwenye msiba ule na kumsaidia Andrew ambaye alionyesha kukata tamaa na alikuwa mdogo sana na baada ya mazishi ndugu wa mama yake waliamua kuwachukua watoto hao na kwenda kuishi nao Moshi, mkoani Kilimanjaro.

## Mzee Regnald na watoto wake watano

HABARI kuhusu familia moja ya Mzee Regnald, alikua na watoto watano, kati ya hao msichana mmoja, kwa bahati nzuri watoto wote walisoma na kupata kazi ila tu msichana hakusoma sana.

Baada ya muda fulani walihamia kijijini kwenda mjini Dar es Salaam huko waliishi muda mrefu hadi mzee Regnald alipofariki ambapo mkewe na watoto walirudi kijijini.

Maisha ya kijijini kwa Mary hayakuwa mazuri ilimlazimu kulaghai wanaume ili apate pesa na kuwa sehemu ya maisha yake, aliendelea hivyo hadi siku moja yalipomkuta pale alipoambukizwa ukimwi.

Ndugu zake walipotambua hilo walikuwa na uwezo wakati huo kulikuwa hakuna dawa za kupunguza makali ya virusi vya ukimwi (ARV) hapa nchini, walimuagizia kutoka nje ya nchi, ambapo alizitumia na afya yake kurejea kama kawaida.

Alianza kuvizia tena wanaume wa watu na kila aliyekuja kwake akumkatalia, watu kijiini walijua ameathirika lakini bado wanaume walimfuata.

Katika pilikapilika hizo alibahatika kupata watoto wawili wa kike, mtoto wapili alipokuwa darasa la pili mama yake alipata mkanda wa jeshi ambao ulimpata usoni na kumlazimu mtoto wake mdogo kumuhudumia kwa muda wa miezi sita alipona na kuingia mtaani tena.

Wanaume wengi kijijini walianza kuumwa, kufa wakimuacha Mary akidunda na hadi mauti yanamfika alishaambukiza wanaume wengi.

Baada ya kifo chake mtoto wake wa kwanza akaanza tabia ya uhuni kama mama yake na kupata ujauzito akiwa kidato cha pili ikambidi kuacha shule ili atunze mtoto.

Kwa sasa hali ya familia hairidhishi, bibi yao amezeeka na hawezi kuwalea wajukuuu na ndugu hawashughuliki, pia watoto hawajui baba zao ni kina nani, basi hiyo ndio hali ya familia hii inayoishi kwa kudra za Mwenyezi Mungu.

## Msichana Salome

KULIKUWA na msichana mmoja jina lake alikuwa anaitwa Salome,alikuwa anaishi na wazazi wake pamoja na kaka yake ambaye anaitwa Frank ambao kabila lao ni Wasukuma.

Kaka yake alikuwa anafanyakazi, siku moja Wazazi wao walipata safari ya kwenda Mwanza kuwasalimu wazazi wao yaani bibi na babu yake Salome.

Wakiwa njiani kwenda Mwanza walipata ajali na wote walifariki pale pale, Salome alilia sana kwa kupoteza wazazi wake wawili.

Baada ya msiba kaka yake Salome alianza kumnyanyasa, alikuwa anampiga hadi anazimia, siku moja Frank alipanga njama ya kwenda kumbaka dada mmoja ambaye bado hajaolewa, kwa kuwa Salome alikuwa na huruma alipojua aliende kumwambia yule dada juu ya njama iliyopangwa.

Siku hiyo Salome alipigwa mpaka akaamua kutoroka na kwenda kuomba kazi katika nyumba moja yenye watoto wawili wa kiume na kike, ambapo mtoto wa kike alikuwa akikaa na wazazi wake huku wa kiume akiwa shule ya bweni.

Baada ya miezi kadhaa kupita baba mwenye nyumba alianza kumtaka Salome kimapenzi, ambapo alikataa suala hilo kwa kuwa anajitambua lakini baba yule aliendelea kumsumbua kiasi cha kufikia hatua ya kumtishia maisha.

Salome aliendelea na msimamo wake, siku moja majira ya saa 7 usiku baba yule bila aibu alimfuata chumbani na mara baada ya kuhisi kitu ndani ya chumba chake alishtuka na kukutana macho kwa macho na bosi wake, alishikwa na butwaa hakujua afanye nini kwa kuwa ilikuwa usiku sana na pia aliogopa kama mke wa bosi

*Inaendelea Uk. 9*

## VIJANA TUONGEE! ANTI SUZY YUPO KUWASIKILIZA NYIE



**"Iwapo una tatizo lolote kuhusu mabadiliko ya mwili wako, afya yako, shule, matatizo ya kifamilia na hata marafiki tafadhali mwandikie Mpendwa Anti Suzy."**

Mpendwa Anti Suzy,
Ni kwa nini vijana wanapenda sana kufanya ngono wakati wa miaka 15 hadi 20 kuliko umri mwingine?
**Anthony**
**Kigonigoni Sec School**

*Si kwel hata kidogo kwamba vijana wa kike na kiume wanapenda kufanya ngono katika umri huo kuliko umri mwingine. Ukweli ni kwamba katika kipindi cha umri huo, vijana wanakuwa wanapata mabadiliko ya kimwili hivyo wanakuwa wadadisi na wanapenda kujaribu mamb ili kuyajua vizuri maumbile yao. Mabadiliko haya mwilini yanasababisha ongezeko la vichocheo, hivyo wanahitaji zaidi kupata taarifa sahihi kuhusu maumbile yao ili kujiepusha na kujiusisha na vitendo vya ngono zisizo salama katika urmi hu mdogo. Kwa taarifa zaidi kuhusu elimu rika wasiliana na mwalimu wako wa ushauri.*

Mpendwa Anti Suzy
Tatizo langu ninapokuwa shuleni darasani nipo makini sana kumsikiliza mwalimu na anapotoa zoezi huwa napata vizuri, lakini kwenye mtihani wa nusu muhula au mwishoni mwa mwaka huwa napata matokeo mabaya. Tafadhali nisaidie anti nifanyeje?
**John**
**Kihurio Sec School**

*Pole sana John kwa tatizo lako hilo na pia napenda kukupa ongera sana kwa kuwa makini dasani tunaitaji vijana wengi wenye mwenendo kama wako kwa maendeleo ya taifa hili. Tatizo la kutofaulu mitihani inawezekana na wewe kuwa woga na hofu unaposikia mithiani hali inayoufanya usahau kila kitu ulichosoma. Nakushauri ujiamini amini ya kuwa unaweza kufauli mithihani na ona mitihani kama zoezi la kawaidaa linalopima uwezo wako kimasomo na Mungu atakusaidia utafaulu.*

Mpendwa Anti Suzy
Mimi ni mwanafunzi wenye umri wa miaka 16, napenda kuuliza kuwa ni kweli kwamba mtu mwenye Virusi vya Ukimwi dalili mojawapo anapoamka anakuwa na utandu mweupe pembeni mwa mdomo wake?
**Asha**
**Ngujini Sec School**

*Jamani mdogo wangu, si kweli kwamba mtu mwenye Virusi vya Ukimwi dalili mojawapo anapoamka anakuwa na utandu mweupe pembeni mwa mdomo wake. Njia sahihi ya kumjua mtu mwenye virusi vya Ukimwi ni kwa kupima pekee na si kutumia macho yetu kupima wengine.*

Mpendwa Anti Suzy,
Mimi ni msichana wa umri wa miaka 17, Je! Kuangalia movie za X zinaweza kumalizia mtu hamu ya kufanya mapenzi? Na je, zinaweza kumkinga mtu asijiingize kwenye ngono? Maana wanasema eti ukiangalia hamu ya kufanya mapenzi huisha.
**Zainabu**
**Kwangu Sec School**

*Si kweli hata kidogo ya kuwa ukiangalia movie za X zinaweza kukupunguziahamu ya kufanya mapenzi badala yake zinakuongezea kwa kiasi kikubwa hamu ya kufanya tendo la kujamiiana. Kwani picha hizo huamsha hisia kubwa sana kiasi cha kukufanya utamani kufanya tendo hilo, njia hii si salama kwani inaweza kukupelekea kwanye ngono zembe.*

*Kuna njia nyingi za kupunguza hamu za kujamiiana ambazo ni salama, kama mazoezi ikiwemo kucheza mpira, kuruka kamba, kubadilishana mawazo na rafiki zako, kujisomea vitabu na hata kutafuta kazi ya kufanya unapohisi unawaza mawazo ya ngono.*

## VIJANA TUONGEE! ANTI SUZY YUPO KUWASIKILIZA NYIE

Mpendwa Anti Suzy,

Mimi naitwa Paul nasoma kidato cha kwanza , nina shida inayonisumbua sana hivi ni kwa nini kila nikisimama na msichana na hata katika maongezi ya kawaidamara ghafla nakuta nimelowanisha nguokwa kutokwa na manii?

**Paul**
**Vudee Sec School**

*Pole sana kwa tatizo linalokusumbua Paul. Napenda kukufahamisha ya kuwa kusimama na msichana sio sababu y wewe kulowanisha nguo yako kwa maniiila hii inatokana na wewe kuwa na mawazo ya ngono sana kichwani mwako kila unapomwona msichana. Jitahidi kutafuta jinsi njingine salama ya kupunguza mawazo hayo yasiyo salama, wewe bado mdogo sana na ndo kwanza upo kidato cha kwanza jitahidi kuelekeza mawazo yako kwenye masomo ngono ni njia isiyo salama kwa kijana kama wewe inaweza kukupelekea kupata maambukizi ya magonjwa ya zinaa au Ukimwi. Jikinge na jitahidi kumwona msichana kama mwanafunzi mwezako.*

Mpendwa Anti Suzy

Mimi ni kijana wa umri wa miaka 19, nasoma kidato cha nne, swali langu ni kwamba: iwapo itatokea kwa bahati mbaya mtu akala mbu ambaye ametoka kufyonza damu ya mtu mwenye virusi vya Ukimwi je, mtu huyo aliyemeza mbu anaweza kupata maambukizi ya Virusi vya Ukimwi?

**Lilian**
**Kindoroko Sec School**

*Mdogo wangu, si kweli hata kidogo mtu huyo hawezi kupata maamdukizi ya virusi vya ukimwi. Kwani mbu hana mfumo wa damu wa kumfanya Kirusi wa ukimwi hastahimili kuishi, virusi vya ukimwi vinaishi kwenye mfumo wa damu wa binadamu pekee na mnyama kama sokwe kwani nae anafanana kikaribu na binadamu. Ndo mana hata mbu akimuuma mtu mwenye virusi vya ukimwi alafu akamwuma mtu mwingine haambukizwi, daima tukumbuke njia kuu za maambukizi ya Ukimwi ni kwa Ngono Zembe, kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na kushirikiana vitu nvenye ncha kali na mtu aliyeathirika.*

Mpendwa Anti Suzy,

Nina swali ambalo kila wakati ndo limekuwa mjadala mtaani kwetu na bado halijapata jibu. Eti ni kweli ukiwa unapiga punyeto kila siku baadaye inaweza kuleta madhara gani?

**Frank**
**Jitengeni Sec School**

*Punyeto ni mojawapo ya njia salama ya kujikinga na ngono zembe hivyo yastahili kuitwa nono salama. Ni salama kwa sababu inaweza kukuepusha na mimba zisizotarajiwa, maambukizi ya magonjwa ya zinaa na VVU. Kuna imani nyingi potofu zinazosambazwa kuhusu punyeto lakini hakuna hata mojawapo iliyothibitishwa kuwa kweli. Punyeto inapigwa na wasichana kwa wavulana ni kitu cha kawaida sana na inachangia kwa kiasi kikubwa katika kuondoa msongo wa mawazo na kupunguza hamu ya kufanya mapenzi, ila tukumbke kila kitu kina kiasi.*

*Namalizia kwa kusema, imekuwa kitu cha kawaida sana kwa vijana weng wa kitanzania sana sana wanafunzi wa shule kijiingiza katika ahusiano ya mapenzi wakati tupo shuleni. Lakini mwanafunzi yoyote aliye makini na anafahamu umuhimu wake kwa kamii jake akiwa kama msomi hawezi kujihusisha na maswala ya mapenzi wakati bado yupo shuleni badala yake atakuwa mstali wa mbele kuielimisha jamii kutambua madhala ya ngono zembe katika kueneza VVU.*

*Napenda sana kuwashauri wasichana wenzangu mlio ashuleni kukumbuka daima kusema HAPANA kwa ukari bila aibu wala woga, tukumbuke kuwa haya ni maisha yetu tunayoyachezea. Tujitambue na kukumbuka kusema NO tusikubali kuburuzwa wala kudanganywa kufanya maamuzi yasiyo sahihi.*

***Asanteni.***

**...Visa na Mkasa vinaendelea...**

*Inatoka Uk. 6*

angejua. Yule baba bila aibu alimbaka na kuondoka akifurahi kwa ushindi huku Salome akilia kwa uchungu mwingi.

Kesho yake walipokea mgeni ambaye Salome hakumjua,ambapo alitumwa dukani kununua soda, na alikwenda haraka na kurudi na kisha kuendelea na kazi zake, akiwa jikoni aliweza kusikiliza maongezi yaliyokuwa yakiendelea baina ya mgeni na mama mwenye nyumba.

**Mgeni:** Mnaendelea kuzitumia zile dawa!!

**Mama Mwenye Nyumba:** Ndio! Tunaendelea kutumia

**Mgeni**: Mnajua hizo dawa hazihitaji mzaha yaani ukiacha Dozi ndio umeharibu kila kitu.

**Baba mwenye nyumba:** Ni kweli unachosema!!

**Mgeni:** Halafu muwe mnatumia kondomu wakati wote wa Kujamiiana au kushiriki tendo la ndoa mana UKIMWI Ni hatari," aliongea kwa msisitizo.

Mungu wangu! Salome alishtuka akiwa na wasiwasi yaani huku akijiuliza wenyewe ina maana yule mgeni ni daktari na hawa wazazi wameathirika kwa UKIMWI? alizana kulia na kuwakumbuka marehemu wazazi wake na baada ya mgeni kuondoka alikusanya vitu vyake na kisha kuwafuata mabosi zake.

**Salome:** Mmeamua kunifanyia hivi? Ili mniambukize UKIMWI au sio (aliongea huku akilia kwa uchungu)

**Mama Mwenye Nyumba:** Hivi wewe una matatizo gani leo? Hayo ndio maneno ya kuongea? Umeanza kiburi?

Salome aliendelea kunung'unika "sawa ndio mmeamua hivyo wewe na mume wako" yule mama aliuliza kwani kuna nini? Salome mbona sio kawaida yako?...Salome alijibu "Mume wako kanibaka halafu nimesikia mmeathirika kwa hiyo sina sababu ya kuendelea kuishi hapa! (Salome aliondoka huku akimuacha mama mwenye nyumba akiwa anashangaa).

Salome alikwenda moja kwa moja hospitalini na baada ya kupima alikutwa ni mjauzito na ana virusi vya UKIMWI,alilia kwa uchungu sana kwani hakuwa na sehemu ya kukaa wala kulala na kuishia kwenye majalala.

Salome alijifungua watoto mapacha baada ya kupata msaada kutoka kwa mama mmoja ambaye alikuwa anapita eneo la jalala na kumpeleka hospitalini,ambapo kutokana na umri wake kuwa mdogo na kutokwa na damu nyingi alifariki muda mfupi baada ya kujifungua.

Yule msamaria kuona vile alikimbia na baada ya uchunguzi wa madaktari watoto walibainika hawana virusi vya UKIMWI, uongozi wa hospitali ulitangaza kwenye vyombo vya habari juu ya watoto hao na mama yao lakini hakuna aliyejitokeza na mwishowe waliamua kuwapeleka katika kituo cha kulelea watoto yatima cha Msimbazi.



*Wanafunzi wa Mvure Sekondari*

# MAANGAMIZI YA UKIMWI

**Na Bestiner Voster**

**Kindoroko Sekondari**

HISTORIA ya familia ya Bwana George ilitokea pindi nilipokuwa darasa la tano mpaka darasa la saba, familia hiyo ya baba na mama na watoto watano ikiwa ni wavulana wawili na wasichana watatu ilikuwa jirani zetu.

Baba na mama walikuwa wanaishi na virusi vya ukimwi, mtoto mkubwa wa familia hiyo aliitwa Suzy na wazazi wake walimsomesha hadi kidato cha nne. Mvulana wa pili kuzaliwa hakufanikiwa kusoma kwani alikataa shule baada ya kujiunga kwenye makundi mabaya.

Bwana George alijishughulisha na kilimo pamoja na ufugaji, kwani licha ya afya yake kudhoofu lakini alifanyakazi kwa bidii na kutimiza mahitaji ya msingi ya familia yake.

Mama Suzy alikuwa Mkuu wa shule ya msingi katika kijiji chao, alifanyakazi kwa bidii na wakati wote alikuwa mcheshi na mwenye kuijali familia yake.

Kwangu mimi nilipokuwa darasa la tano ndio nilianza kusikia habari za ugonjwa wa Ukimwi na nilikuwa najiuliza ukimwi ni nini? Kwani nilisikia watu wakizungumza juu ya ukimwi.

Kadri tulivyoendelea kuishi nilijifunza kutoka kwenye hiyo familia licha ya kwamba sikujua kama ndio ukimwi halisi ninaosikia, wazazi wa ile familia walikuwa wakishikwa na homa za mara kwa mara, ngozi inabadilika kuwa yenye mabaka, kukohoa mara kwa mara, nywele kubadilika na kuwa wakali sana unaweza kuogopa wakati mwingine.

Niliwaonea huruma sana lakini kulingana na mapenzi ya Mungu mtoto wao wa kwanza alikuwa ameelimika na hivyo aliitunza familia na hata baba alipofariki.

Ah! Familia ikabakiwa na mama wakaendelea kuishi vizuri tu,mama ndio akawa mwenye kubeba majukumu ya familia, yule mama alikuwa mvumilivu sana katika kukabiliana na matatizo yake.

Baada ya miaka miwili alianza kuumwa sana ambapo aliuguzwa na kufarijiwa na watoto wake pamoja na ndugu na marafiki lakini baadaye alifariki.

Suzy na wadogo zake walikuwa na uchungu mwingi huku akijiuliza ataishije bila wazazi na wadogo zake nani atatimiza mahitaji ya msingi?

Mbaya zaidi kulingana na ukoo ulivyopanga mali za wazazi wao ziligawanywa kwa watoto ikiwa ni pamoja na baadhi ya watoto kulelewa na ndugu wa baba na mama.

Ni kweli kuwa UKIMWI ni hatari sana katika maisha yetu kwani umesababisha uwepo watoto wa mitaani, yatima, umeleta umaskini na utengano wa watoto.

Kwa hiyo tunatakiwa kulinda afya zetu kwa hali na mali kuepuka tamaa za mwili na anasa, kuepuka ngono zembe, kuchangia vifaa vyenye ncha kali, kuepuka damu isiyo salama.

Kupima afya baada ya miezi mitatu na kuwa mwaminifu katika ndoa, marafiki pamoja na kuwa wazi na wakweli katika maisha ya ndoa na maisha tunayoishi kila siku.




*Huduma ya upimaji wa hiyari ni muhimu kwa wananchi kujua hali za afya zao.*

# TUBADILIKE!

**Na Gift Joseph**

**Kindoroko Sekondari**

KIJANA mmoja kwa jina Brighton Anthony mkazi wa wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam alikuwa akiishi na wazazi wake (Baba na Mama), mwenendo wake wa maisha haukuwa mzuri jambo ambalo halikuwa furahisha wazazi na waliamua kukaa naye na kuzungumza na kumuonya juu ya tabia yake na kumpa wosia wa mambo aliyokuwa akiyafanya.

Wakati anafanya hayo tayari alikuwa amemaliza elimu ya msingi na hakuweza kuendelea na masomo ya sekondari kutokana hali duni kwenye familia yao.

Brighton akiwa na wazazi wake alikuwa akijishughulisha na shughuli mbalimbali mtaani ikiwemo kibarua cha ujenzi ambacho kilikuwa kikimpatia mahitaji yake ingawa ilikuwa haitoshelezi.

Baada ya miaka mitatu kupita alimpa ujauzito msichana mmoja ambapo taarifa hizo ziliwafikia wazazi wake ambao hawakuweza kuchuka hatua zozote kwa kuwa mtoto wao hakuwataarifu kuhusiana na jambo hilo, kadri siku zilivyozidi kwenda na mimba iliendelea kukua na ndipo wazazi wa msichana walipoamua kuvunja ukimya na kumuuliza mtoto wao ambaye aliwaeleza muhusika ni nani na ndipo walipoamua kumpeleka kwa kina Brighton.

Kwa kuwa wazazi wa kijana huyo walikuwa na taarifa za jambo hilo hawakushtuka sana, hivyo ikawabidi wachukue hatua ya kwenda nyumbani kwa yule binti kwa ajili ya kujitambulisha na kutoa mahari.

Baada ya miezi michache Brighton aliamua kujitegemea kwa kupanga chumba, lakini kutokana na kipato finyu alishindwa kumchukua mke wake ili waishi pamoja licha ya mkewe kutaka waishi pamoja lakini alijitetea kuwa hali yake kiuchumi si nzuri kwa kuwa hakuwa na kazi maalum ya kumuingizi kipato.

Brighton alikubali wakaanza maisha ya pamoja lakini kadri siku zilivyozidi kusonga ndivyo maisha yao yalivyozidi kuwa magumu na ndipo alipoamua kwenda kujifunza udereva akiamini ipo siku atafanikiwa.

Mungu hakuwa mbali naye kwani alipoanza kazi maisha yake yalibadilika na kuweza kumudu mahitaji ya msingi ya familia yake na baada ya muda walijaliwa mtoto wa kiume na kumuita Chrispin.

Baada ya maisha ya Brighton kubadilika na tabia yake ilibadilika pia, kwani alianza kutokuwa mwaminifu kwa mkewe na kuanza kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi na wanawake wengine kiasi cha kutorudi nyumbani na alikuwa akijihusisha na mapenzi na mama mmoja ambaye inasemekana hakuwahi kuolewa wala kuwa na mtoto na badala yake kujihusisha kwenye mapenzi na vijana wadogo ikiwa ni pamoja na kutumia imani za kishirikina katika kuwapata.

Brighton aliitelekeza familia yake, ambapo mke wake alifikisha malalamiko kwa wakwe zake ambao walimuita na kumuonya lakini hakusikia na kuendelea na tabia hiyo na wakati huo huo yule mama aliye na mahusiano naye aliposikia malalamiko hayo alianza kumtolea maneno ya vitisho ikiwa ni pamoja na kumpiga kila wanapokutana.

Baada ya mke wa Brighton kuona maisha kwake yamekuwa magumu aliamua kuanzisha biashara ndogo ya kuuza maandazi ili kupata fedha za matumzi kwani wakati huo mumewe aliacha kutoa hata fedha za matumizi na mahitaji ya msingi ya familia, yule mama bado aliendelea kumsumbua na wazazi wa Brighton hawakuwa na cha kufanya kwa kuwa walimuonya mara nyingi hakusikia, mwishowe waliamua kuihudumia familia ya mtoto wao.

***Inaendelea Uk. 12***

*Inatoka Uk. 12*

Habari zikaenea kuwa yule mama alikuwa anaishi na Virusi vya Ukimwi lakini Brighton hakujali, siku, miezi ilipita ndipo Brighton alianza kupata magonjwa ya mara kwa mara na afya yake kudhorota na ndipo baba yake alimshauri aende kupima.

Kijana yule alikana na kusema hawezi kuwa na virusi vya ukimwi hadi wazazi wake walipomchukua kwa nguvu na kwenda kumpima ambapo majibu yalionyesha kuwa ana virusi vya ukimwi huku kinga yake ya mwili (CD4) ikiwa imeshuka sana na hivyo kutoa nafasi kwa mwili kushambuliwa na magonjwa nyemelezi.

Brighton alianzishwa dawa za kurefusha maisha (ARV), wakati akiendelea kutumia dawa hizo aliugua sana kichwa na shingo yake kukakamaa na aliporejeshwa hospitalini daktari alimueleza kuwa hali hiyo inasababishwa na kukosa lishe bora kwani dawa hizo zinahitaji lishe na kufuata masharti.

Wazazi wake waliamua kwenda kumpima mkewe na mtoto na kubainika kuwa hata mkewe ameathirika lakini mtoto alikuwa mzima.

Mke wake alilia sana kwani alikuwa akimuonya mumewe juu ya tabia zake na ndipo naye alipoanza kutumia dawa.

Wazazi wake walishindwa kuamini na kuelewa kuwa mtoto wao anaishi kwa matumaini lakini hakukua na jinsi na ndipo walipokubaliana na hali halisi na baadaye kuizoea na kuona ni ya kawaida.

Brighton alibadilika kabisa na kuwa mtulivu kwa mke wake na ndivyo hadi leo wanaishi kwa matumani na wapo mkoani Arusha.



*Picha ya wanafunzi wa shule ya sekondari Kindoroko iliyopo wilayani Mwanga mkoani Kilimanjaro*

# Utafiti wa Ugonjwa wa Ukimwi na Virusi (HIV/AIDS CASE STUDY)

**Na Bakari Ramadhani, Jitengeni Sekondari**

Mimi ni mwanafunzi wa shule ya sekondari Jitengeni Kihurio,nipo kidato cha tatu mkondo wa biashara na sasa nina umri wa miaka 17, ninayo masikitiko makubwa kwani wazazi wangu wote walifariki kwa ugonjwa wa ukimwi tangu nikiwa darasa la saba.

Jambo hilo lilisababisha mimi na mdogo wangu kuishi maisha ya shida kwani mahitaji muhimu ya shule tuliyakosa kama vile madaftari na kalamu na hata matokeo yetu ya darasa la saba kuwa mabaya na kulazimika kwenda shule binafsi ili kujiendeleza.

Baada ya kufariki kwa wazazi wetu wawili ilitubidi mimi pamoja na mdogo wangu tuishi na baba mdogo mpaka sasa ambaye anatusomesha kwa kipato kidogo anachopata kutokana na mauzo ya mpunga.

Pamoja na kwamba baba ananilipia ada lakini haitoshelezi kwani analipa kiasi tu na hivyo wakati mwingine kufukuzwa shule kwa kushindwa kulipa ada.

Si hayo tu, lakini pamoja na matumizi mengine ya shule kama kalamu na madaftari, kwa sababu hii huwa mimi pamoja na mdogo wangu tunafanya kazi za vibarua angalau tuweze kupata fedha za kikidhi mahitaji yetu.

Pamoja na hayo yote kuna mahitaji mengine kama chakula ili tuweze kusoma kikamilifu, kwani chakula hakina ubora unaotakiwa.

Mahitaji mengine kama vile sehemu ya kulala ni tatizo na hii hutupelekea kulala chini kwa kutumia magunia kwani baba mdogo hana uwezo wa kununua godoro kwani hata chakula chenyewe kinampa shida, ikiwa ni pamoja na kutokuwa na umeme na hivyo kusoma kwa kutumia kibatari.

Pia, tunapatwa na matatizo ya mara kwa mara ya kiafya kama vile kukohoa, malaria na mafua na hii ni kwa sababu tunalala chini, lakini hatua hata fedha za matibabu.

Kwa ujumla matatizo haya yamesababisha mimi na mdogo wangu kushindwa kufanya vizuri katika masomo yetu,kwani muda mwingi tunautumia katika kufanya kazi ambazo baadhi zimezidi umri wetu na hivyo kupata matatizo ya kifua kwa kuwa na maumivu makali, pia baada ya kurejea kutoka kwenye kazi hizo huwa tunachoka sana na hivyo kushindwa hata kujisomea.

Sina mengi bali hayo ndio naona yanafanya maisha kuwa magumu kwani ninapambana na majukumu ambayo yapo nje ya uwezo wangu.



*Wanafunzi wa shule ya sekondari Jitengeni wakiwa katika picha ya pamoja na mwalimu wao.*

# Wasemavyo wanafunzi baada yakuhojiwa na walimu

**Na Ruben Ruben na Julian Mjema**

MAKIHIO ni msichana ambye alikuwa anaishi katika kijiji cha Kihurio wilayani Same mkoani Kilimanjaro, baba yake alikuwa anaitwa Zawadi na mama yake alikuwa anaitwa Nampenda na pia alikuwa na wadogo zake wawili wa kike.

Familia yao ilikuwa duni sana. Makihio alikuwa ndiye msichana pekee katika familia yao aliyefanikiwa kuendelea na masomo ya sekondari hadi kidato cha nne.

Wazazi wake ingawaje walikuwa maskini lakini walifanya kila mbinu na kuhakikisha kwamba mtoto wao anamaliza shule.

Hatimaye Makihio alimaliza shule (Kidato cha nne) na matokeo yake yalikuwa mabaya kwani alipata daraja la sifuri (divison 0).

Wazazi wake walisikitika sana kwani mtoto wao ambaye walimtarajia kuwa mwokozi (Mkombozi) wa maisha yao. Maisha ya familia yao yalizidi kuwa magumu katika hali ambayo ilichangia kumsukuma Makihio kujiingiza kwenye mapenzi.

Siku moja katika kuzunguka zunguka Makihio alikutana na mvulana aliyejitambulisha kwa jina la Mberwa Mashambo. Mvulana huyo alikuwa anampenda sana Makihio lakini Makihio hakumpenda kwa sababu alikuwa maskini. Siku iliyofuata akatokea mvulana mwingine ambaye alikuja kwa mtindo mwingine na alijitambulisha kwa jina la Mkwizu Selanyika ambaye alikuwa anatoka katika familia ya kitajiri. Mkwizu alikuwa ni anaishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) na hakutaka kubainisha hali hii.

Makihio hakuchelewa kutoa majibu kwani alikubali bila kufikiria kwamba ingekuaje baadaye. Mkwizu na Makihio walikubalina na kupanga wakutane kwenye nyumba ya kulala wageni. Huko walifanya ngono zembe iliyosababisha Makihio kuambukizwa virusi vya ukimwi (VVU) bila ya yeye kujua.

Hapo awali Makihio hakuwa na desturi ya kufanya ngono na wala hakuwa na mpenzi na mara alipoanza kufanya ngono kwa mara ya kwanza Mkwizu alionekana kuwa na hali ya wasiwasi na hatimaye baada ya miezi miwili ndipo akaamau kwenda kupima na kujua afya yake kama ni salama au la?

Kabla ya kupima mshauri nasaha alimuuliza Makihio moja ya swali lifuatalo, Je kwanini umeamua kuja kupima VVU? Alijibu: "Nimeamua kupima kutokana na wasiwasi uliojaa moyoni mwangu kwani hapo mwanzoni sikuwa na mpenzi wala desturi ya kufanya tendo lakini sasa nina mpenzi na nimeshaanza kufanya tendo la ndoa tena bila kutumia kondomu."

Baada ya hapo Makihio akachukuliwa damu kwa ajili ya vipimo na hatimaye majibu yalitoka na kuonyesha kuwa ameathirika na virusi vya ukimwi (VVU).

Makihio alihuzunika sana na hakusita kumueleza mpenzi wake (Mkwizu) ila Mkwizu hakuonyesha hali yoyote ya huzuni bali aliangusha kicheko cha kejeli na kumwambia Makihio kwamba "Ulichokuwa unakitaka umeshakipata na kuanzia sasa sikutaki tena," kauli hiyo ilimfanya Makihio kugundua kwamba chanzo cha hali yake ni Mkwizu.

Makihio alionekana kuwa na huzuni wakati wote na hata wazazi wake waligundua hilo na wakaanza kumpekua na hatimaye Makihio akawaeleza hali halisi ya afya yake kwamba ni muathirika wa virusi vya ukimwi (VVU). Wazazi wake hawakuamini kwani waliogopa sana kusikia hayo,amani ndani ya nyumba ikaanza kuvurugika.

Kadri siku zilivyozidi kwenda wanafamilia walianza kumfanyia Makihio vitendo vya ajabu sana kwa sababu yeye ni muathirika wa VVU.

Familia yake ilianza kumtenga na kumnyanyapaa kwa maneno na vitendo,walimtengea vyombo vyake peke yake na hakuruhusiwa kushiriki meza moja na wanafamilia wakati wa kula.

***Inaendelea Uk. 15***

*Inatoka Uk. 14*

Vile vile marafiki waliokuwa wakimpenda walimkimbia na hawakutaka kushirikiana naye katika mambo mbalimbali ya kimaisha.Makihio alifadhaika sana moyoni mwake na afya yake alizidi kudhoofika bila kupata msaada wowote katika familia yake na marafiki zake.

Makihio alijuta moyoni mwake na kusema kwamba ni heri angemkubali yule kijana maskini (Mberwa) ambaye pengine afya yake ilikuwa nzuri kuliko Mkwizu aliyemuambukiza virusi vya ukimwi kwa makusudi.

Pia Makihio akasema ni heri asingekuwa wazi juu ya hali yake ya kuishi na virusi vya ukimwi (VVU) pengine asingetengwa na kunyanyapaliwa na watu ikiwemo familia yake.



*Wanafunzi wa shule ya Kihurio ambao wamepatiwa elimu ya masuala ya ukimwi.*

## Wanafunzi wanahitaji Elimu inayofaa



***Makala hii imeandaliwa na Mwalimu Rajabu Omari wa Shule ya sekondari Jitengeni ambaye amekuwa akitoa elimu ya Ukimwi shuleni humo.***

KWA kiasi kikubwa elimu ya ukimwi tunayotoa kwa wanafunzi chini ya ufadhili wa shirika lisilo la kiserikali la SMECAO (Same and Mwanga Environmental Conservation Advisory Organization), imesaidia kwa kiasi kikubwa wanafunzi kujitambua.

Wanafunzi tunawafundisha kujikinga na njia za kuzuia maambukizi ikiwa ni pamoja na namna ya kuishi na wale wanaoishi na watu wenye virusi vya ukimwi bila kuwanyanyapaa kwani ni kinyume kabisa.

Kwa takribani miezi mitano sasa wanafunzi wetu wanapewa elimu kila wakati na wengi kwa sasa wanauelewa mkubwa wa masuala ya ukimwi na hilo tumelibaini kwani kabla ya kuwapa elimu tulifanya tathmini na baada ya kuwapa elimu tulifanya tathmini na kubaini kuwa elimu waliyopewa imewaingia na wanaweza kuitumia katika maisha yao ya kila siku na jamii yao kwa ujumla.

Ili elimu hii iwe endelevu ni vyema wanafunzi wakapatiwa vijarida na vipeperushi vya masuala ya ukimwi ili waweze kuendelea kupata elimu na kujifunza mambo mapya yanayotokea katika jamii nyingine nchini.

Ukimwi ni janga la kitaifa na limesababisha kushusha uchumi wa taifa, kuongeza watoto wa mazingira magumu na yatima, utegemezi katika familia na kushusha kipato cha familia moja moja.

Ni wajibu wa jamii kushiriki kwa vitendo katika mapambano dhidi ya virusi vya ukimwi na kutochukulia jambo hilo kwa mzaha huku asilimia kubwa ya Watanzania wakiendelea kuteketea.

# Same and Mwanga Environmental Conservation Advisory Organization (SMECAO)



Jarida hili hutolewa na
SMECAO FUND,
P.O BOX 87,
SAME - KILIMANJARO,
Email: smecao@gmail.com,
smecao@elct.org,
Website: www.smecao.jimdo.com